



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Kumb.Na. AC.209/366/02'C'/13

Tarehe: 09/02/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kutokana na kibali cha Ajira chenye Kumb. Na. FA.170/521/01'B'/29 ya tarehe 14 Januari, 2021 kuhusu ombi la kibali cha ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora (OR-UTUMISHI).

Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia waombaji wote raia wa Tanzania wenye sifa na uwezo kuomba nafasi moja (1) ya kazi ya Msaidizi wa Kumbukumbu II

MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II - NAFASI (1)

Ngazi ya Mshahara ni TGS B₁ sawa na shilingi 390,000/= kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Cheti cha Kuhitimu kidato cha IV na VI.
- Cheti cha Astashahada (Technician Certificate – NTA LEVEL 5) cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

MAJUKUMU YA KAZI

- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka /mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- Kuthibiti upokeaji, uandakishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu, nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala /vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu (barua , nyaraka nk) katika mafaili.

MASHARTI KWA UJUMLA

- I. Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45 awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.
- II. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- III. Mwombaji aambatanishe taarifa zake binafsi (CV) ikionyesha sanduku la posta, E-mail namba za simu anazotumia na uzoefu wake kazini.
- IV. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato channe (IV) au sita (VI), cheti cha kuzaliwa na Picha 2 (passport size) za hivi karibuni.
- V. Mwombaji anatakiwa aambatanishe Vyeti vilivyo sainiwa na kupigwa mhuri (CERTIFIED COPY) wa Mwanasheria au Mahakama.
- VI. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 24/02/2021 saa 9:30 alasiri aidha maombi yote yawasilishwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 352,

NYANG'HWALE

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri

www.nyanghwaledc.go.tz na katika mbao za matangazo.


DAVID T. RWAZO

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NYANG'HWALE

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
NYANG'HWALE DISTRICT
P. O. Box 352
GEITA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita,
Barua pepe: ded@nyanghwaledc.go.tz Tovuti: www.nyanghwale.go.tz